

Wataalamu wengi wametoa hoja kwamba hakuna matumizi ya teknolojia moja peke yake ambayo yanaweza kuboresha kilimo cha Afrika. Badala yake, wanapendekeza kwamba wakulima watumie mbinu mbalimbali zinazopatikana katika anuai za mifumo ya kilimo


Kama mbadala wa kilimo kikubwa cha aina moja ya zao, taratibu za kilimo ekolojia zinasaidia kuimarisha afya ya udongo na rutuba, uzalishaji endelevu wa chakula na kuongeza kipato cha mkulima. Mbinu hizo zinajumuisha:

- kupumzisha shamba – kuiacha ardhi bila kuilima ili irudishe rutuba baada ya kipindi fulani;
- kuozesha mbolea ya samadi na ile ya vunde kwenye shimo;
- kuongeza matamahuluku - inajumuisha udongo wa kichuguu cha mchwa, mbolea ya mifugo na majani yaliyooza;
- kuchanganya mazao ya nafaka na mikunde kama vile njungu mawe na mbaazi;
- kutengeneza virutubisho vya nitrojeni;
- kilimo mzunguko – kwa mfano, nafaka, karanga na miti ya jamii ya mikunde (*faidherbia albida*);
- kilimo misitu – mchanganyiko wa miti, mazao na mifugo; na
- mifumo inayoungwa mkono ya anuai za mbegu zinazosimamiwa na mkulima.

Taratibu za sasa za kilimo ekolojia zinifuata misingi ya utendaji ya kilimo cha asili iliyochanguliwa kwa muda mrefu na wakulima wa Afrika. Mbinu hizo ni za wakulima, ambao ni lazima wajumuishwe katika mchakato wa tafiti na maendeleo yanayowagusa.

WAKULIMA WANA MBADALA

WA UTARATIBU WA MAPINDUZI YA KIJANI



duducoelio.com